HALMASHAURI YA MJI WA IFAKARA

HOTUBA YA MKURUGENZI KATIKA MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA HALMASHAURI YA MJI IFAKARA

Wakuu wa Idara na Vitengo, Watumishi wa Halmashauri mliohudhuria leo, **Amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yenu**.

Ndugu Watumishi, kama mnavyofahamu kila Mwaka Nchi yetu huadhimisha maadhimisho ya wiki ya Utumishi wa Umma ambayo hufanyika kila Mwaka kati ya Tarehe 16 ya Mwezi Juni na Tarehe 23 ya Mwezi Juni na huratibiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Maadhimisho haya ni moja ya matukio yaliyopo katika kalenda ya Umoja wa Afrika (AU) ambapo Nchi wanachama huadhimisha kila Mwaka kwa kufanya Maonesho na kuelezea kazi zao mbalimbali, lengo kuu likiwa kutambua mchango wa Watumishi wa Umma katika utoaji wa huduma kwa wateja ili kuleta Maendeleo ya Taifa letu.

Ndugu Watumishi, kauli mbiu ya Maadhimisho haya kwa Mwaka huu ni:
"KUIMARISHA USHIRIKISHWAJI WA JAMII KATIKA UTOAJI HUDUMA, VIJANA WASHIRIKISHWE KULETA MABADILIKO BARANI AFRIKA"

Hapa Halmashauri ya Mji wa Ifakara tunafanya maadhimisho haya kwa masuala yafuatayo:

1. Kukutana na ninyi Watumishi kwa kuwasikiliza kero zenu na kushughulikia kero mbalimbali
2. Kuhimiza Watumishi kufanya kazi kwa bidii na kwa kiwango cha juu ili kuongeza tija na ufanisi katika kazi

Ndugu Watumishi, nilitoa utaratibu wa Watumishi kuwasilisha kero/maoni yao kwa maandishi lakini mpaka leo kero ziliwasilishwa ni….. ambazo zitatolewa ufafanuzi hapo baadae. Watumishi wenzangu naelewa kabisa kuwa kwa siku ya leo tu hatuwezi kukamilisha kero zote na maoni tuliyonayo juu ya mustakabali wa Halmashauri yetu na Serikali kwa ujumla na kero ambazo hutolewa na wateja wetu na jinsi ya kuzitatua, hivyo basi kila Mtumishi ambaye atakuwa hajapata nafasi ya kutoa kero yake leo au kero zinazotolewa mara nyingi na Wateja tunaowahudumia alete suala/kero yake Ofisi ya Mkurugenzi pale kwa Katibu Muhtasi au kwa Afisa Malalamiko Bwana Michael Danga Ofisi ya Mipango kabla au ifikapo tarehe 28/06/2017 kwa ajili ya kushughulikia na kuandaa taarifa.

Ndugu Watumishi, kabla sijatoa nafasi kwenu ya kutoa ya kuwasilisha kero/ushauri/maoni/maswali nina masuala kadhaa ya kuwaambia Watumishi wenzangu.

Kwanza kabisa kulingana na kauli Mbiu ya Mh. Rais wetu ya **HAPA KAZI TU** mnatakiwa kuitekeleza kwa Vitendo kwa kufanya kazi kwa bidii, watumishi mjitume, muwajibike na mfuate kanuni, taratibu na sheria za kazi mfano kuacha tabia ya utoro na ubadhirifu mbalimbali, na kutumia muda wa kazi vizuri kwa kuwahi na kutoa huduma vizuri kwa Wateja na kufuata utaratibu wa ruhusa pale inapobidi kutokuwepo kazini, kwani kutokuwepo kituoni/kazini bila taarifa ni kosa kwa mujibu wa kanuni za kudumu za utumishi wa umma, tusiwasumbue wateja bila sababu za msingi hivyo kwa kifupi kauli mbiu hii inatakiwa tuitekeleze kwa vitendo. Watumishi wote tunatakiwa tufanye kazi kwa pamoja 'team work' katika vituo vyetu vya kazi.

Pili ni suala la uhakiki wa vyeti vya shule na taaluma ambavyo viko chini ya Baraza la Mitihani (NECTA) ambalo linaendelea na naendelea kupata taarifa zingine kuhusu walioghushi au vyeti vyao vyenye utata hivyo tuendelee kutoa ushirikiano katika hili ili kuweza kuwa na Watumishi wa Halmashauri wenye sifa na vigezo vinavyotakiwa. Katika uhakiki huu Halmashauri imepoteza Watumishi 22, ambao watumishi 14 Ni wa Idara ya Elimu Msingi, Watumishi 6 Idara ya Afya, Mtumishi 1 Idara ya Ujenzi na Mtumishi 1 Kitengo cha Manunuzi. Watumishi 5 ni wenye vyeti vyenye Utata na Watumishi 13. wana vyeti ambavyo havikukamilika hivyo wanatakiwa kuwasilisha vyeti vyao ambavyo hawakukamilisha.
Ndugu Watumishi, zoezi la uhakiki wa vyeti bado linaendelea na muda si mrefu Maafisa Utumishi wote watapatiwa mafunzo juu ya kuhakiki taarifa zenu za NIDA na zilizopo katika 'payrol' hivyo mshiriki kikamilifu mara mtakapotangaziwa kuhusu zoezi hilo muhimu.

Tatu, suala la usafi wa Jumamosi ya kila ya mwisho Mwezi, Mh. Rais aliagiza kuwa kila jumamosi ya mwisho wa Mwezi iwe ni siku ya usafi Kitaifa, hivyo nasisitiza kuwa ninyi kama Watumishi wa Umma muwe kioo cha usafi na kujitokeza katika kufanya usafi huo ili kuweka mazingira safi. **Nawaagiza Wakuu wa Idara na Vitengo kusimamia Watumishi walio chini yenu juu ya suala hilo.**

Nne, Watumishi mnatakiwa muwe na mahusiano mazuri katika kazi, nawashauri muwe mnakutana kila Mwezi mnakaaa vikao vya Idara/Vitengo kushauriana juu ya utekelezaji wa shughuli zenu na kupanga mikakati ya kutoa huduma kwa wateja.

Tano, Watumishi mna haki ya kudai stahili zenu na mna wajibu wa kuwajibika ipasavyo. Stahili ziwe za bila udanganyifu kwani wapo watumishi wanaomba malimbikizo ya Mishahara mara mbili au tatu na wamegundulika hivyo walilipa kwa mkupuo, wapo wanaoghushi mahala pa asili (place of domicile), vyeti vya ndoa na vyeti vya kuzaliwa watoto, huo si uadilifu na ikigundulika hatua kali za kinidhamu na za kughushi zitachukuliwa dhidi yako. Hivyo nasisitiza tuwe waadilifu.

Sita, tumetoa masanduku ya maoni katika kila Ofisi za Kata, masoko, na Hospitali pia tuna dawati la malalamiko hivyo nawashauri kutumia masanduku na dawati hilo vizuri ili kuweza kupata maoni mbalimbali na kero na ziweze kutatuliwa kwa wakati kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni.

Saba, Serikali imezindua mfumo mpya wa malipo ya mishahara ambapo kuanzia Mwezi Julai 2017 mishahara itakuwa inalipwa moja kwa moja kupitia Benki kuu hivyo Watumishi wote muhakikishe majina yenu ya kwenye 'payrol' yanaendana na majina ya akaunti zenu benki mnapopokelea Mshahara. Wahusika wa kubadilisha majina katika Akaunti ni Banki na wahusika wa kubadilisha majina katika taarifa ya mishahara ni Ofisi ya Mkurugenzi, Idara ya Utumishi kwa kutumia mfumo wa 'HCMIS- LAWSON'. Pia nawakumbusha mjenge tabia ya kufatilia usahihi wa taarifa zenu has aza majina, umri na vyeo husika.
Ndugu Watumishi, suala la hati za mishahara kuanzia Mwezi Julai zitakuwa haziletwi kutoka hazina hivyo kutakuwa na utaratibu wa Mtumishi mwenyewe kupata hati ya Mshahara (salary slip) kupitia tovuti itakayoanzishwa na hazina ambayo haitakuwa tofauti na hati ya mishaharaa iliyokuwa ikitolewa awali.

Nane, makato ya mikopo ya elimu ya juu kwa sasa ni asilimia 15% badala ya 8% ya awali, hivyo bodi inakusudia kila Mtumishi ambaye alinufaika na mkopo huo na bado hakatwi awasilishe majina yake kamili idarani kwake ili majina hayo yatumwe Bodi ya Mikopo, hivyo taarifa hizo za ambao hamjaanza kukatwa lakini mlinufaika zifike Idarani kwenu kabla au ifikapo Tarehe 10 Julai 2017. **Nawaagiza Wakuu wa Idara na Vitengo kusimamia Watumishi walio chini yenu juu ya suala hilo**

Tisa, Watumishi wanaokaribia kustaafu na wengine mnakumbushwa kufanya maandalizi mapema, taarifa zinatakiwa zifike katika mfuko wa Jamii unaochangia miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu. Hii ni pamoja na kujenga utaratibu wa kuomba taarifa za michango yenu. Aidha muiandikie Ofisi kupatiwa kibali cha kustaafu mapema kwa ajili ya maandalizi.

Kumi , Halmashauri kwa sasa ina tovuti yake ambayo ni www.ifakara.go.tz ambapo utapata taarifa mbalimbali za uendeshaji wa Halmashauri na utapata nafasi ya kutoa maoni juu ya uboreshaji wa Halmashauri, lakini pia tovuti hii inalenga kurahisishautoaji huduma kwa kuwapatia maelekezo na fomu mbalimbali, hivyo tutumie tovuti hii vizuri. Pia hata hotuba yangu hii utaipata kwenye tovuti ya Halmashauri.

Kumi na moja, Halmashauri ya Mji inaendelea na mchakato wa utekelezaji wa upimaji wa viwanja 2900 ambapo katika mradi huu viwanja 900 vitapimwa kwa kushirikiana na Kampuni binafsi na viwanja 2000 vitapimwa kwa kushirikiana na Unit Trust of Tanzania Project Infrastructures (UTT-PID) katika kata za Michenga na Kibaoni.

Ndugu Watumishi, utekelezaji wa mradi huu ni kwamba katika upimaji wa viwanja 2000 Unit Trust of Tanzania Project Infrastructures (UTT-PID) ilifika katika Halmashauri ya Mji tarehe 14 Machi 2017 kwa ajili ya kutembelea maeneo ambapo mradi huu utafanyika, UTT iliridhika na maeneo hayo. Mradi huu utaanza wakati wowote mwezi wa saba.

Halmashauri imepeleka barua kwa wadau mbali mbali wa ndani na nje ya Mji wakiwemo watumishi wa Halmashauri ya Mji kuwaomba kuonyesha nia ya kununua viwanja vitakavyopimwa kutokana na mradi huo, Aidha watumishi watakaokuwa na sifa za kukopesheka watakopeshwa viwanja kupitia mishahara yao na wasio kuwa na sifa watalipia pesa taslimu kwa awamu kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Utaratibu wa namna wa kufanya malipo/dhamana (Security deposit) ambayo ni 50,000 kwa mtu binafsi na 500,000 kwa Kampuni utawekwa hapo baadaye. **Hivyo watumishi wenzangu wito wangu kwenu ni kwamba tutumie fursa hii adhimu kwa ajili ya kuonesha nia ya uhitaji wa viwanja hivyo katika maeneo tajwa kwa ajili ya ustawi wa maisha yetu.**

Ndugu Watumishi, baada ya kusema hayo, nawatakia wiki njema ya maadhimisho, tufanye kazi kwa bidii na kujituma kwa maendeleo ya Halmashauri yetu na Taifa kwa ujumla, nawashukuruni sana na nawakaribisha kwa kutoa kero, maoni, ushauri na malalamiko.

"Ushiriki wangu, Jukumu langu pamoja tuijenge Ifakara yetu"